


ENE LA OFISI:

Family Intervention Program (FIP)
(Family Safety Center)
610 Murfreesboro Pike
Nashville TN 37210



Programu ya Kusaidia Familia (FIP) ipo kwenye Kituo cha Usalama wa Familia. Unapowasili, jisajili kwa walinzi.




Kwa miadi piga
(615) 862-7773

Mradi huu ulitegemezwa kwa Tuzo Na. 2017-VA-GX-0051 ilituzwa na Ofisi kwa ajili ya Wahanga wa Uhalifu, Ofisi ya Programu za Haki, Idara ya Haki ya Marekani kupitia Ofisi ya Programu za Sheria ya Uhalifu ya Tennessee.

Swahili

KUREJESHA MAISHA
JINSI YALIVYOKUWA



"Njia bora zaidi ya kushinda jambo ni kukabiliana nalo"

Mwandishi Hajulikani



"Yaliyopita na yanayokuja ni mambo madogo ukilinganisha na yaliyo ndani mwetu"

Ralph Waldo Emerson



PALE WEWE AU MTU UNAYEMJUA ANAPOATHIRIWA NA UHALIFU

Kila wakati uhalifu unapotokea, watu wengi wanaathirika — mhanga, wanafamilia, rafiki na hata jumuiya nzima. Hakuna mtu anayejiandaa kwa maumivu ya kimwili na kihisia yatokanayo na uhalifu ambayo yanaweza kuwa na madhara makubwa kwa wale wanaoumizwa na kwa familia na rafiki zao. Baada ya kuguswa na mateso ya watu ambao maisha yao yanaathiriwa na uhalifu, Idara ya Polisi ya Metropolitan Nashville (MNP) inatoa huduma za ushauri, utetezi, na usaidizi kwa wahanga wa uhalifu na watu wengine ambao maisha yao yanaathiriwa na uhalifu wa kikatili tangu mwaka 1975.

MSAADA UMEFIKA

Mwaka 2016, programu mbili za MNP za ushauri na utetezi, Programu ya Kusaidia Wahanga (VIP) na Kutoa Ushauri wa Ukatili wa Majumbani ziliunganishwa na kuwa Programu ya Kusaidia Familia (FIP). Huduma hizi zilijengwa juu ya dhana kwamba yeyote anayepitia mfadhaiko kutokana na tendo la kihalifu anapaswa kupewa usaidizi wa bure na wa haraka wa janga na ufuatiliaji. Ikiwa na wataalamu wa afya ya akili wenye leseni, na wanasheria mahiri, FIP imedhamiria kuwasaidia wale wanaoathiriwa na ukatili, kutafuta na kurejeza hali ya amani na usawaziko kwenye maisha yao. Uamuzi wa mhanga kuhusu mashtaka hauathiri ustahili wa huduma. Dhima ya FIP ni kutoa huduma za afya ya akili na utetezi wa masuala ya kisheria kila wakati watu, familia, na/au jamii inapoathiriwa na uhalifu wa kikatili. Huduma zote ni bure, za siri, na zinatolewa katika mazingira ambayo yanaunga mkono tofauti za kitamaduni: kwa kuzingatia mbari, dini, imani, na jinsia.



HUDUMA MBALIMBALI

Wafanyakazi wakarimu na wanaozingatia tamaduni wanatoa:

USAIDIZI WA JANGA

Mwitikio wa haraka wa saa 24 kwa wahanga na raia, kutoka kwa maafisa husika, pale uhalifu unaporipotiwa.

USHAURI

Ushauri wa kitaaluma kwa watu binafsi, wanafamilia na watu wengine wanaoathirika na uhalifu. Makundi ya usaidizi kwa wahanga/almanusura yanatolewa katika kipindi chote cha mwaka.

MWITIKIO WA JANGA LA KIKUNDI

Usaidizi wa janga la kikundi unatolewa kwa ombi pale biashara, shule, au vikundi vingine vinapoathirika na uhalifu.

UTETEZI NA USIMAMIZI WA MASHAURI

Mwongozo, usaidizi, na ufafanuzi kuhusu taratibu zote za kipolisi na kimahakama. Usaidizi unapatikana kwa ajili ya kupata mahitaji muhimu na kujaza fomu ya Fidia ya Majeraha ya Uhalifu ya Tennessee.

HUDUMA MAALUM

Utetezi/ufikiaji unaozingatia masuala ya utamaduni kwa watu tofauti wa Nashville wakiwemo wataalamu wakimbizi na wahamiaji, wafanyakazi wanaoongea lugha mbili, taarifa katika lugha mbalimbali, na matumizi ya wakalimani wanapohitajika.

USHAURI NA MAFUNZO

Huduma za uwasilishaji zinapatikana kwa makundi ya jumuiya na wanataaluma ili kuongeza utambuzi na uelewa wa huduma za FIP, madhara ya mfadhaiko/dhuluma; na utambuzi wa masuala ya kitamaduni na uzingatiaji kwa makundi mahsusi ya wahanga.

TAARIFA NA RUFUA

Uratibu pamoja na watoa huduma za afya, huduma za jamii na masuala ya kisheria.

NI UAMUZI WAKO

Lengo kuu ya Programu ya Kusaidia Familia ni kusaidia watu binafsi na wapendwa wao kurejea katika hali ya afya na ustawi baada ya kutokewa na janga fulani. Ikiwa wewe au mtu unayemjua ni mhanga wa uhalifu, tafadhali piga simu stahiki iliyoorodheshwa hapo chini.

Programu ya Kusaidia Familia (615) 862-7773

NAMBARI NYINGINE ZA MAWASILIANO

Upelelezi wa Polisi:

Kanda ya Kaskazini	(615) 862-7901
Kanda ya Kusini	(615) 862-7763
Kanda ya Mashariki	(615) 862-7525
Kanda ya Magharibi	(615) 862-7385
Kanda ya Midtown Hills	(615) 880-1513
Kanda ya Hermitage	(615) 862-6993
Kanda ya Madison	(615) 880-3311
Kanda ya Kati	(615) 862-7044
Kitengo cha Uhalifu wa Kingono	(615) 862-7540
Idara ya Ukatili wa Majumbani	(615) 880-3000
Ofisi ya Mwanasheria wa Wilaya	(615) 862-5500
Fidia ya Majeraha ya Uhalifi ya Tennessee	(615) 741-2734

REJEA PANELI YA NYUMA KWA RAMANI NA MAELEKEZO.



(615) 862-7773